

**Elimu ya Afya ya Uzazi**  
**Utafiti wa Sera na Utekelezaji**  
**Shule za Msingi na Sekondari**  
**Tanzania Bara**

**Muhtasari**

**Novemba 2021**





# 1. Utangulizi

Kama sehemu ya juhudi za kutetea haki na elimu ya mtoto wa kike, Mwaka 2021 HakiElimu ilifanya utafiti kutathmini elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika shule za msingi na za sekondari Tanzania Bara. Mapendekezo ya kufanya utafiti huu yalitokana na kubainika mapungufu kwenye sera, miongozo na utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia, kwa vijana balehe. Mapitio ya machapisho mbalimbali yalionyesha uwepo wa athari kwa wavulana na wasichana ambao hawakupata elimu ya afya ya uzazi wakati waumri balehe – hasa katika shule za msingi na sekondari.

Tangu Mwaka 2021 kumekuwa na juhudi jumuisi za kuunganisha elimu ya haki ya afya ya uzazi na jinsia shuleni, kupitia mtaala wa elimu ya jinsia katika programu ya kuboresha elimu kwa waalimu. HakiElimu, tumeamua kufanya utafiti huu ili kubaini kama elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia imejumuishwa kwenye mfumo rasmi wa shule, kama afua ya kimkakati ya kuwafikia vijana tangu wakiwa na umri mdogo, hivyo kupunguza vitendo hatarishi vyenye athari kama vile magonjwa ya zinaa, ukimwi/VVU, pamoja na mimba zisizotarajiwa.

## **2. Madhumuni ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuchunguza uzingatiaji wa haki ya elimu ya afya ya uzazi katika mfumo wa elimumsingi Tanzania Bara.

### **2.1. Hususan, utafiti ulilenga kuchunguza kuhusu:**

- Uwepo wa Sera, sheria na miongozo mahsusi ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika shule za msingi na sekondari.
- Maudhui ya mtaala juu ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika ngazi ya shule za msingi na sekondari.
- Ufundishaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika shule za msingi na sekondari nchini Tanzania.
- Mchango wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika kuboresha upatikanaji wa elimu kwa wasichana.

### 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanyika kwa kutumia mbinu mchanganyiko za kupima ubora na takwimu zenye maelezo. Utafiti ulifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Lindi, Rukwa, Mara na Arusha. Mikoa ilichaguliwa kwa lengo la kupata uwakilishi wa maeneo yenye idadi kubwa na idadi ndogo vya matukio ya mimba za utotoni, kwa mujibu wa takwimu za Utafiti wa Taifa wa Kidemografia na Hali ya Afya-Viashiria vya Malaria (TDHS-MIS) wa Mwaka 2015/2016.

**Jedwali 1: Idadi za mimba za utotoni katika mikoa iliyoshiriki kwenye utafiti**

Mkoa	Idadi za mimba za utotoni kimkoa	Idadi za mimba za utotoni kikanda
Dodoma	39%	32%
Lindi	28%	28%
Rukwa	29%	34%
Mara	37%	29%
Arusha	15%	15%

*Chanzo: TDHS-MIS 2015/2016*

Utafiti huu ulihusisha makundi mawili; kundi la vijana balehe/vijana na kundi la watu wazima. Kundi la vijana balehe/vijana lilihusisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19. Kundi la watu wazima lilihusisha wakuu wa shule, wahudumu wa afya, waalimu, wawakilishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Maafisa Elimu wa Mkoa na Wilaya, taasisi za mafunzo ya waalimu, mashirika yasiyo ya kiserikali/asasi za kiraia na wadau wengine wa kisekta.

## 4. Matokeo ya Utafiti

### 4.1. Uwepo wa sheria na miongozo ya ufundishwaji wa haki ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni

Machapisho mbalimbali yanaonesha kwamba Tanzania inasimama kidedea miongoni mwa nchi zenye Sera na sheria zinazoruhusu upatikanaji wa Haki ya Elimu ya Afya ya Uzazi, licha ya mapungufu yaliyopo. Hizi ni pamoja na:

#### Miongozo katika Sekta ya Elimu

- Sheria ya Mwaka 1978 ya Elimu ya Taifa, imerekebisha Mwaka 1995
- Sera ya Elimu na Mafunzo (2014)
- Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (ESDP), 2016/17-2020/21.
- Ripoti ya Mwaka ya Utendaji wa Sekta ya Elimu (AESP)

#### Miongozo katika Sekta ya Afya (inayohusiana na Sekta ya Elimu)

- Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya (HSSP) V, 2020-2025
- Mpango wa III wa Afya ya Uzazi, Watoto Wachanga, Watoto na Vijana Balehe, ambao unajilikana pia kama Mpango Mmoja wa Tatu (One Plan III) 2020-2025;
- Sera ya Taifa ya Afya (2007) na Kanuni ya Adhabu (Penal Code), Sura ya 16 (RE 2002)
- Mkakati wa Taifa wa Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (ADHD) (2018)<sup>1</sup>

1 MoHCDGEC (2018) National Adolescent Health and Development [https://tciurbanhealth.org/wp-content/uploads/2017/12/020518\\_Adolescent-and-Development-Strategy-Tanzania\\_vF.pdf](https://tciurbanhealth.org/wp-content/uploads/2017/12/020518_Adolescent-and-Development-Strategy-Tanzania_vF.pdf)

- Mpango wa Kitaifa wa Ajenda ya Kuchochea Uwekezaji kwa ajili ya Afya ya Vijana (National Accelerated Action and Investment Agenda for Adolescent Health and Wellbeing – NAIA-AHW)

Hata hivyo, utafiti unaonyesha utofauti kwenye uelewa miongoni mwa wadau mbalimbali kuhusu Sera, sheria na miongozo iliyopo, hivyo kusababisha changamoto kwenye utekelezaji wake, hususan, namna elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inavyotolewa shuleni. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa Sera na miongozo inayohusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia ni pamoja na; mifumo hafifu ya uratibu wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia, kutokukidhi mahitaji ya vijana balehe, na uelewa mdogo na ushiriki hafifu wa watekelezaji muhimu kama vile maafisa elimu na maafisa wa afya. Kwa ujumla, dhana ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inaonekana zaidi katika Sera za Afya kuliko katika Sera za Elimu.

## **4.2. Utekelezaji wa miongozo ya Sera, mitaala na sheria kuhusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia nchini Tanzania**

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Mwaka 2012, vilibainika vikwazo vikubwa vitatu katika utekelezaji wa Sera na miongozo juu ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia:

- Ukosefu wa mitaala yenye ufanisi na vifaa vya kufundishia/kujifunzia juu ya elimu ya kina ya jinsia (59.7%);
- Ukosefu wa taarifa kuhusu upatikanaji wa huduma za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia (41.1%); na
- Miongoni mwa wahudumuwa afya wapo ambao hawana kiwango cha kutosha cha stadi zinazohitajika kwa ajili ya kutoa elimu ya jinsia (56.5%).

Utafiti huu pia ulibaini uwepo wa vikwazo vifuatavyo vya ziada; uhaba wa rasilimali, miundombinu duni ya kufundishia/kujifunza, upinzani kutoka kwa vikundi shinikizi kama vile viongozi wa dini na viongozi wa kimila, utashi dhaifu wa kisiasa na uongozi kukabiliana na uhalisia wa mahitaji ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kwa kizazi cha sasa.

### **4.3. Namna elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia ilivyozingatiwa katika mitaala ya elimumsingi**

Walipohojiwa kuhusu namna ambavyo elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia ilivyochopekwa kwenye mtaala wa shule:

- Asilimia 46.7 ya washiriki walisema kupitia masomo ya sayansi
- Asilimia 36.7 walisema kupitia ‘program maalum’ kama vile vipindi vya kujenga uwezo vinavyotolewa na waalimu na wanajamii.

### **4.4. Maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yaliyomo kwenye masomo ya shule za msingi na sekondari**


Machapisho yalionyesha kwamba:

- Katika shule za sekondari, maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yameingizwa katika somo la Biolojia (94.1%), Uraia na Maadili (16.2%), Sayansi na Teknolojia (11.3%)
- Katika shule za msingi, maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yameingizwa kwenye somo la Sayansi na Teknolojia (95.7%), Uraia na Maadili (28.5%) na kwenye Biolojia (1.9%).

Utafiti huu umebaini kuwa maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shule za msingi ni ya kiwango cha chini ya wastani, kama ilivyoelekezwa kwenye Kielelezo Na1.




**Kielelezo 1: Asilimia ya wanafunzi waliotaja mada mbalimbali za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia zinazofundishwa shule za msingi**



*(Chanzo: Takwemu za utafiti, 2021)*

Katika shule za sekondari maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika mada au masomo yalikuwa asilimia 50% zaidi ya maudhui hayo katika shule za msingi.

**Kielelezo 2: Asilimia ya wanafunzi waliotaja mada mbalimbali za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia zinazofundishwa shule za sekondari**



*(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)*

#### **4.5. Kukidhi kwa maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika mtaala**

- Kwa mujibu wa matokeo, asilimia 15 ya wanafunzi walisema kwamba maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yanatosheleza.
- Asilimia 93.3 ya waalimu waliohojiwa walisema kwamba maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia hayatoshelezi.
- Asilimia 33.3 ya waalimu waliohojiwa walisema kwamba maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia hayafai kwa wanafunzi japokuwa wanafunzi waliona kwamba mada zote haziwafai.

#### **4.6. Namna ambavyo maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yanavyoendana na mtaala wa shule**

Elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inazingatiwa kuwa ni muhimu na inafaa kwa kuwapatia wanafunzi maarifa na stadi za kuepuka madhara yanayotokana na vitendo vyao, ikiwemo mimba zisizotarajiwa na maambukizi ya magonjwa.

*“Binafsi, naona elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia ni nzuri kwa sababu inakuza uelewa miongoni mwa vijana balebe kuhusu masuala ya afya ya uzazi, kujibeshimu na kujilinda. Hii inawasaidia wanafunzi kuepuka mimba wakiva shuleni na kuwa na tabia hatarishi. Wanafunzi pia wanawasaidia wenzao kufikia malengo yao” [Afisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia].*


#### **4.7. Udhaifu wa maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika mtaala wa shule**

Maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yanapatikana zaidi katika mtaala na masomo ya madarasa ya juu. Hii inawafanya wanafunzi

katika madarasa ya chini kukosa maarifa muhimu, kwani wavulana na wasichana wengi wanabalehe mapema, wakiwa katika madarasa ya chini.

- Asilimia 73 ya waalimu waliohojiwa wanaamini kwamba elimu ya jisia na afya ya uzazi inapaswa kutolewa kuanzia Darasa la IV, hasa kwa wanafunzi waliofikia umri wa miaka 10 hadi 12.
- Wastani wa asilimia 81.65 ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanapendelea kupata elimu ya haki za ujinsia na afya ya uzazi wakiwa shule za msingi.

**Kielelezo 3: Asilimia ya wanafunzi waliotoa mapendekezo kuhusu kipindi kizuri cha kuanza utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni**



*(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)*

## 4.8. Kukidhi kwa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kulingana na mahitaji ya wanafunzi

Uchambuzi ulionyesha matokeo mchanganyiko:

- Takriban asilimia 30 ya waalimu waliohojiwa walisema kwamba elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inatosheleza, inakidhi mahitaji ya wanafunzi na inaweza kutolewa kwa watoto wenye

umri wa miaka 10.

- Takriban asilimia 40 ya waalimu walisema kwamba elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inakidhi mahitaji ya wanafunzi lakini inapaswa itolewe kwa watoto wenye umri kuanzia miaka 12.
- Chini ya asilimia 30 waliona kwamba elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia haikidhi mahitaji ya wanafunzi.

#### **4.9. Maeneo ya kuboresha katika mchakato wa utoaji elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia**

Utafiti unapendekeza uboreshaji katika maeneo makuu manne:

- Elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia itolewe kama somo linalojitegemea .
- Wahudumu wa afya washirikishwe kwenye ufundishaji na uelimishaji wa afya ya uzazi na haki za jinsia kutokana na utaalumu wao.
- Upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia uboreshwe kuhakikisha wanafunzi wanajifunza elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kwa ufasaha.
- Maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia yaboreshwe ili kuendana na mabadiliko ya mfumo wa maisha na maendeleo ya ulimwengu.

#### **4.10. Kiwango cha kuridhika kwa wanafunzi kwenye ufundishaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni**


- Wanafunzi wa shule za msingi wanaridhika kwa asilimia zaidi 92.8 na mada zilizopo kwenye elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia na namna zinavyofundishwa kuliko wale walioko shule za

sekondari (80.4%).

#### 4.11. Sababu za kuridhika na ufundishaji wa mada za zinazohusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia

Utafiti umebaini sababu mabli mbali zinazopelekea wanafunzi kuridhika na elimu ya afya ya uzazi kama inavyoelezwa hapo chini.

**Kielelezo 4: Sababu za kuridhika na namna ambavyo mada za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia zinavyofundishwa**




*(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)*

#### 4.12. Sababu za kutoridhika na ufundishaji wa mada zinazohusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia

Wastani wa asilimia 13.38 ya washiriki kwenye shule za msingi na sekondari walisema kwamba, hawaridhishwi na namna ambavyo mada za

afya ya uzazi na haki za jinsia zinavyofundishwa.

**Kielelezo 5: Sababu za kutoridhika na ufundishwaji wa mada za afya ya uzazi na haki za jinsia**



(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)

### 4.13. Changamoto katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni

- Mtazamo hasi wa baadhi ya waalimu na maafisa ambao wana wasiwasi kwamba elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia itachochea tabia potofu kwa vijana balehe.
- Ukosefu wa mazungumzo ya wazi yanayohusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kwenye ngazi ya familia.
- Mila na desturi potofu zinazochangia madhara kwa baadhi ya jamii.
- Waalimu huona aibu kufundisha baadhi ya mada, hivyo wanafunzi wanaomba wafundishwe na wahudumu wa afya, pia kutenganisha wavulana na wasichana katika madarasa tofauti.

- Elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia haipewi muda na rasilimali za kutosha hivyo haitolewi kwa mwendelezo mashuleni na haipewi kipaumbele katika ufundishaji. Kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia mada hizi.
- Matumizi ya lugha ya Kiingereza kufundisha na kujifunza inawanyima baadhi ya wanafunzi kuelewa, na wakati mwingine hubaki wanacheka tu wakati wa somo.

#### **4.14. Usawa wa ushiriki kwenye ufundishwaji na ujifunzaji wa mada za afya ya uzazi na haki za jinsia**

Pamoja na kwamba walimu wamekubali umuhimu wa ushiriki sawia ya wasichana na wavulana kwenye elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia wapo waliosema kama ifuatavyo:

- Asilimia 49 ya waalimu walisema wanatenganisha madarasa ya wasichana na wavulana wakati wa kufundisha mada afya ya uzazi na haki za jinsia ili wanafunzi wa kike wafundishwe na walimu wa kike na wa kiume wafundishwe na walimu wa kiume.
- Asilimia 30 ya waalimu walipendekeza matumizi ya mbinu mchanganyiko, kwa pamoja au kwa utaratibu wa mbinu moja moja.
- Ni asilimia 20 tu ya waalimu walitaja ushiriki usiolingana wa wavulana na wasichana, wakiwapa kipaumbele wasichana kwa sababu wao wako kwenye kundi hatarishi na wana mahitaji maalum zaidi.
- Takriban asilimia 53 ya waalimu hawajakutana na wanafunzi wenye mahitaji maalum, hata hivyo, waliona umuhimu wa kuwafundisha bila ubaguzi wowote endapo ingetokea.

#### **4.15. Uwezo wa waalimu kutoa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia**

- Takriban asilimia 32 ya wanafunzi walisema kwamba waalimu hawana uwezo wa kutoa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Asilimia 66 ya waalimu, walisema wanao uwezo wa kutosha na wanajiamini kufundisha mada zinazohusiana na afya ya uzazi na haki za jinsia, japokuwa uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja, kuboresha uwezo wao wa kufundisha, vingewasaidia zaidi.
- Asilimia 20 tu ya waalimu walikubali kuwa na uwezo mdogo katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Takriban asilimia 50 ya waalimu waliomba mafunzo ya ziada kutokana na upungufu wa maarifa ya kufundisha afya ya uzazi na haki za jinsia.

#### **4.16. Sababu zinazoathiri umahiri wa waalimu katika kutoa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia**

- Muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya kufundisha mada zenye maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Waalimu kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada za afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Ukosefu wa vifaa vya kufundisha hupelekea wanafunzi kutokuwa makini wakati wa vipindi vya mada zinazohusu afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Takriban asilimia 50 ya waalimu hawakupata mafunzo jinsi ya kufundisha afya ya uzazi na haki za jinsia wakiwa kazini.



- Ni asilimia kama 50 tu ya waalimu waliopata huhudhuria aina fulani ya semina au uboreshaji wa uwezo kwenye utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.

#### 4.17. Huduma za ushauri nasihi kwa wanafunzi

- Asilimia 50 ya waalimu huzungumza na watoto iwapo watakuwa wamebainika kuwa na mienendo mibaya. Hiyo inazingatiwa kama ushauri nasihi.
- Asilimia 80 ya waalimu hawana mafunzo rasmi kwenye utoaji wa ushauri nasihi
- Ni asilimia 20 tu ya waalimu walithibitisha kwamba wamepata mafunzo ya utoaji wa ushauri nasihi.

#### 4.18. Mahali ambapo wanafunzi/watoto hupata taarifa zaidi kuhusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia (Tazama Jedwali 2)

**Jedwali 2: Mitazamo ya washiriki kuhusu chanzo kikuu cha ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia(N=410)**

Chanzo kikuu cha taarifa ya afya ya uzazi	Mtazamo wa washiriki kama wanayo maarifa ya kutosha kuhusu elimu ya afya ya uzazi	
	Ndiyo	Hapana
Vitabu	3 (0.9%)	1 (1.1%)
Kanisa/Msikiti	2 (0.6%)	0 (0.0%)
Baba	15 (4.7%)	8 (8.7%)
Vyombo vya Habari	1 (0.3%)	0 (0.0%)
Mama	71 (22.3%)	24 (26.1%)
Wanafunzi wengine na marafiki	4 (1.3%)	4 (4.3%)
Wengine	8 (2.5%)	1 (1.1%)
Mtoa huduma	6 (1.9%)	1 (1.1%)
Mwalimu	208 (65.4%)	53 (57.6%)

(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)

### 4.19. Ushiriki wa wazazi na jamii kwenye elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia


- Baadhi ya taratibu za kimila na kitamaduni zinazuia ushirikiano kati ya mzazi na mtoto na mazungumzo ya wazi kuhusu elimu ya afya ya uzazi.
- Mtaala wa shule za msingi na sekondari hautoi fursa ya kushirikisha wazazi /walezi katika mchakato wa kufundisha-kujifunza.

### 4.20. Faida za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni

- Asilimia 65 ya waalimu walisema kwamba, elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia huchangia kuongeza fursa za elimu, pamoja na kuboresha matokeo chanya kwenye ufaulu, hususan kwa watoto wa kike.
- Kuongezeka kwa mahudhurio shuleni, kujiamini na kupunguza utoro shuleni.

Kielelezo kilichopo hapa chini kinaonesha mitazamo kuhusu faida ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.

**Kielelezo 6: Faida zilizotajwa kutokana na elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia. (majibu mchanganyiko)**



(Chanzo: Takwimu za utafiti, 2021)

## 5. Hitimisho

Tanzania inazo Sera, miongozo na sheria mbalimbali kuhusu njia za kushughulikia masuala ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kwa vijana balehe na vijana. Hata hivyo, inaelekea kuwa, elimu hii hupatikana kwa shida katika maeneo mbalimbali. Pamoja na kwamba mada za elimu ya afya ya uzazi zimechopekwa katika masomo ya Biolojia, Uraia, Maadili na Stadi za Kazi, upo wasiwasi kuhusu kina cha mada hizo na changamoto katika kufundisha na kujifunza inayopelekea pendekezo la kufanya somo la elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kuwa somo linalojitegemea (yaani lisiunganishwe na masomo mengine). Upungufu wa vifaa vya kufundishia na ukosefu wa mafunzo miongoni mwa waalimu vinaonekana kuathiri utoaji wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia, japokuwa waalimu walisema wanajiamini kufundisha. Elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia inaonekana kuchangia upatikanaji wa elimu kwa wasichana, na ufaulu wa kimasomo. Hivyo, ni muhimu wadau kuendelea kutetea na kuwekeza kwenye elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia nchini, ili kuhakisha kwamba wanafunzi, hasa wasichana na wavulana, wanafaidika na elimu hiyo.

## 6. Mapendekezo

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba, elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia imewaacha wasichana walio katika madarasa ya chini ya shule ya msingi. Kwa kuwa wasichana wengi hubalehe katika umri mdogo, inapendekezwa kwamba, somo hili litolewe kuanzia madarasa ya chini zaidi. Utafiti huu unapendekeza pia kuboresha maeneo yafuatayo ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia Tanzania Bara:

- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine washirikiane kuingiza elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika mifumo na taratibu za Sekta ya Elimu.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine watekeleze kwa pamoja vipaumbele muhimu vilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe (ADHD), hasa ukuzaji wa mtaala kamili wa elimu ya afya ya uzazi.
- Wakati wa kuandaa Mpango mpya wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa kuandaa viashiria vinavyohusiana na ufuatiliaji wa maarifa ya wanafunzi kwenye elimu ya afya ya uzazi na jinsia, kuanzia umri wa miaka 10 hadi 15, kwani baadhi ya vijana balehe huingia kwenye mahusiano ya kujamiiana kabla ya kutimiza miaka 15.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa kuhakikisha kwamba Sera na miongozo inayohusu elimu ya afya ya uzazi zinapatikana katika ngazi ya shule na kwamba waalimu wanao uwezo wa kuvitumia kwa lengo lililokusudiwa.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya,

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine wapitie mtaala wa shule za msingi na za sekondari, na kuiboresha ikilenga zaidi haki za jinsia na maendeleo ya binadamu, mahusiano, elimua ya afya ya uzazi kama sehemu ya stadi za maisha.

- Huenda utafiti wa ziada utahitajika kuelewa matarajio ya waalimu, wazazi na wanajamii kuhusu elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia.
- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa kutoa mafunzo ya lazima kwa waalimu wote wakiwa bado masomoni jinsi ya kufundisha afya ya uzazi na haki za jinsia, pamoja na mbinu za kutoa ushauri nasaha na nasihi.
- Masomo ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika taasisi za mafunzo ya waalimu zinapaswa kuboreshwa ili kuhakikisha waalimu wanaandaliwa vya kutosha na wanao ujuzi wa kufundisha mada za elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia shuleni.
- Jitihada za pamoja zifanyike kuongeza maudhui ya elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia katika rasilimali za kufundishia, kama vile miundo ya via vya uzazi, ili kuhakikisha ufanisi wa elimu ya kina kuhusu wa somo husika.
- Kuongeza upatikanaji wa vifaa vya habari, elimu na mawasiliano ikiwemo majarida, mabango na matangazo kwa ajili ya wanafunzi kufanya rejea.
- Wizara zinazohusika na uratibu wa wahudumu wa afya watoe huduma za ugani kwa watoto wa kiume na wa kike walio ndani na nje ya shule. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itoe matibabu ya bure ya magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya zinaa kwa vijana balehe katika vituo vya afya vya umma.

- Kuanzisha vituo rafiki vya afya kwa vijana
- Kutoa mafunzo kwa vijana, hasa wa kike, namna ya kushona sodo zinazoweza kutumika tena. Vinginevyo, washonaji katika eneo husika wapewe mafunzo ili waweze kushona na kuuza sodo kwa bei nafuu.
- Dawati la elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia lianzishwe kwenye kila shule.
- Wazazi wahamasishwe kwenye kutoa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia na masuala mengine yanayohusiana na hilo.
- Jamii ielemishwe juu ya umuhimu wa elimu ya afya ya uzazi na haki za jinsia kwenye kaya kwa vikundi au mtu mmoja mmoja kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Mapendekezo kama haya yametolewa pia katika tafiti za awali.





**HakiElimu inawawezesha wananchi kufanya  
mabadiliko katika elimu na demokrasia**

P.O. Box 79401, Dar es Salaam, Tanzania

Tel: +255 (0)22 2151852/3 Fax:+255 (0)22 2152449

Email: [info@hakielimu.or.tz](mailto:info@hakielimu.or.tz)

Website: [www.hakielimu.or.tz](http://www.hakielimu.or.tz)

